Msamaha Wa Dhambi Na Hakikisho La Amani Na Mungu

WILLIAM J. PATTON

UTANGULIZI

Msomaji wangu mpenzi,

Kile ninacho nuia katika kijitabu hiki ni kwamba kwa baraka za Mungu, uweze kumpokea Bwana Yesu Kristo kama Mwokozi wako; na ikiwa umeshampokea uweze kujua kwa uhakika kwamba una uzima wa milele.

Nina hamu kubwa kuhusu njia utakayoitumia kukisoma, ili ukaweze kunufaika kwayo.

1. Kisome ukiwa peke yako na Mungu, na sio ukiwa na wengine wakikusumbua.

2. Kisome polepole, Hakuna haja ya kujiharakisha kwa kijitabu kama hiki.

3. Kisome kwa njia ya maombi ukimuuliza Mungu akifanye kuwa ndiyo njia ya kukuelekeza kwa Kristo.

4. Kisome kwa ajili yako na wala sio kwa wengine. Kitumie maishani mwako.

Na kabla hujakimaliza, uweze kusema "Kwa maana namjua yeye niliyemwamini, na kusadiki ya kwamba aweza kukilinda kile nilichokiweka amana kwake hata siku ile." 2 Tim. 1:12

Kijitabu hiki kilitungwa hasa na mapambo kutoka kwa kile kitabu maarufu "Pardon and Assurance" cha Wm J. Patton wa Dromara, Co. Down, N.Ireland.

NI KWA NINI WAKRISTO WANA FURAHA

Na William J. Patton.

Wamesamehewa na kuokolewa; wakati mtu anapoona ya kwamba amemuasi Mungu mara elfu na ya kwamba dhambi zake zinamwelekeza jehenamu. Anapoona ya kwamba Kristo amempenda, na ameichukua adhabu ya dhambi hizo zote, na ya kwamba zimesamehewa na kusahaulika, - je, hataweza kufurahi? Je Mwanamaji anapookolewa toka kwa kaburi ya maji hafurahi?

Msomaji-haungalikuwa na furaha kuu zaidi ukijua ya kwamba dhambi zako zimesamehewa? Kwa sasa hudhubutu kuwaza juu ya kifo, au juu ya hukumu au juu ya jehenamu. Wakati Roho wa Mungu anapoyaleta mambo haya katika mawazo yako, unajaribu kuyafutia mbali. Biblia inasema "Heri mtu yule ambaye dhambi zake zimesamehewa ambaye dhambi zake zimefunikwa".

Mungu anawapenda wakristo nao wanampenda. Ni raha kiasi gani kwa mkristo kujua kwamba anaye Yesu, rafiki huyu mpendwa aliye naye, kila siku na kila saa, kumwongoza, na kumhifadhi na kumtimizia mahitaji yake yote. Mtume Petro alisema kumhusu Yesu:"Naye mwampenda ijapokuwa hamkumwona; ambaye ijapokuwa hamwoni sasa mnamwamini nakufurahi sana kwa furaha isiyoonekana, yenye utukufu."

"Wakristo wana ushirika na Mungu - kuzungumza na Mungu na Mungu Kuzungumza nao. Ni furaha iliyoje Mkristo anapoifungua Biblia na kusema "Nena Bwana Mtumishi wako anasikia." Na je ni furaha kuu iliopo wakati mwingine katika umati mkuu, ukimtukuza na kumhimidi Baba yetu wa mbinguni, au kuketi mezani mwa mwanawe kwa furaha kuu.

Wakristo wana furaha kwa kuishinda dhambi, kwa kumpendeza Mungu, na kwa kuwafanyia wema watu wengine. Biblia inasema "Kwa kuzitii amri za Mungu kuna tunzo kuu." Mkristo anapofanya mambo hayo kumpendeza Yesu Kristo mwokozi wake, ni furaha ya kiasi gani wanayotoa!

NI FURAHA ILIYOJE KUMFANYIA MUNGU KAZI SIKU KUTWA.

Na Mungu anapomfanya Mkristo kuwa njia ya kuongoza roho kwa Yesu, na kisha "kumbadili mwenye dhambi kutoka kwa njia zake mbaya na kuokoa nafsi kutoka kwa mauti inampa furaha mara mia zaidi kuliko kuitosheleza tamaa yeyote mbaya. McCheyne alisema "Ni furaha ilioje siku yote, kumfanyia Mungu Kazi siku yote, na kisha kupumzika chini ya tabasamu yake.

Wakristo wana furaha kwa kutazamia mbinguni kama mji wao wa milele, kuwa daima nyumbani mwa baba, ambapo pana makao mengi. Kuwa mahali ambapo hapana huzuni au maumivu au uchungu. Kuwa milele na Baba ambaye alitupenda na Mwanawe aliyekufa kwa ajili yetu, na kuwa na Roho Mtakatifu ambaye aliyetuleta kwenye shina la msalaba. Kuwa milele na malaika watakatifu ambao wametuzunguka duniani. Kuwa na rafiki zetu wapendwa waliolala ndani ya Yesu.

Wakristo wana furaha ndani ya kifo. Kifo ni Bwana Yesu akija na Kuwachukua nyumbani kwake. Payson, alipokuwa akifa alisema; "Mji wa mbinguni umejaa maoni yangu. Utukufu wake hung'aa juu yangu, upepo wake wanipepea, na roho yake imepuliziwa rohoni mwangu."

UPENDO WA KRISTO KWA WENYE DHAMBI

Katika Luka 15, Yesu anajieleza mwenyewe kama Mchungaji mwema, aliyeenda kumtafuta kondoo mmoja aliyepotea hadi akampata. Kisha akamweka juu ya mabega yake akifurahi na akawaita marafiki zake kufurahi pamoja naye. Kwa maana alimpata kondoo aliyepotea. Ah, ya kwamba ungemruhusu akubebe mabegani mwake leo! Angefurahi, na angewaita malaika wafurahi pamoja naye. Luka 15:10.

Upendo wa Yesu kwa mwenye dhambi ulionekana katika maisha yake duniani. Yeye aliyekuwa na mfano wa Mungu, kwa ajili yetu alijifanya asiye na sifa, akajichukulia mfano wa mtumwa, akazaliwa

na bikira, na akawa na umbo la mwanadamu. Hebu na tukumbuke ya kwamba ndiye Yesu. "Yule yule jana, leo na milele".

Tazama yule mwanamke aliyekuwa mwenye dhambi akija kwa Yesu (katika Luka 7). Aliiosha miguu ya Yesu kwa machozi yake, na kuipanguza kwa nywele za kichwa chake. Yesu hakumtupilia mbali, mbali alisema "Dhambi zake, zilizokuwa nyingi zimesamehewa" Mwanamke huyu mwenye dhambi ambaye alikuwa ametoka katika dhambi zake na kumgeukia Yesu, alisamehewa bure kwa neema yake.

Pia tazama Zakayo yule mtoza ushuru na mnyanganyi. Alipanda juu ya mkuyu kwa maana alitaka kumwona Yesu akipita. Yesu alitazama juu na kusema "Zakayo shuka chini, leo wokovu umefika katika nyumba yako" Zakayo alishuka chini na kusema" "Tazama bwana, cho chote nilichochukua kwa njia isiyo ya haki kutoka kwa yeyote nitamrudishia mara nne ne nusu ya mali ya kitakachobaki nitawapa masikini." Hapo pana ushahidi ya kwamba roho yake ilikuwa imebadilika na dhambi zake kutupiliwa mbali. Na Yesu yu ngali yule leo.

LEO UTAKUWA PAMOJA NAMI PARADISO

Tazama Yesu katika siku yake ya kufa. Baada ya kumsulubisha msalabani aliomba "Baba wasamehe kwa maana hawajui watendalo". Ajabu moja siku hiyo ilikuwa ni kuokolewa kwa mwizi aliyekuwa akifa, ambaye aliomba "Bwana nikumbuke utakapofika katika ufalme wako" Jibu la Yesu kwa haraka lilikuwa "Amini amini nakwambia hivi leo utakuwa pamoja nami katika paradiso". Asubuhi mtu huyo alikuwa katika dhambi zake; adhuhuri aliokolewa na Kristo; jioni alikuwa na kristo paradiso. Alihesabiwa haki, akatakaswa na akafanywa tayari wa mbinguni katika masaa machache. Oh ni neema ya Bwana Yesu kwa watu wambaya!

Tazama Yesu kailvari, alikufa kwa ajili ya akina nani? Kristo hakufa kwa ajili ya watu wema, bali kwa wasio wema. Warumi 5:6 Biblia yasema "Bali alijeruhiwa kwa makosa yetu. Alichimbuliwa kwa maovu yetu: na kwa kupigwa kwake sisi tumepona. Na bwana ameweka juu yake maovu yetu sisi." Isaiah 53:5,6.

Yesu azibeba dhambi zetu na mwili wake juu ya mti. 1 Petro 2:24. Mateso juu ya mwili wake masaa hayo yaliyokuwa ya kuumiza mno, lakini mateso yake makuu yalikuwa yale ya nafsi yake. Akawa dhambi kwa ajili yetu, yeye asiyejua dhambi. Na kwa ajili ya dhambi zetu alizowekelewa yeye. Baba yake akauficha uso wake kutoka kwake hadi alipolia "Mungu wangu Mungu wangu mbona umeniache?" Oh upendo wa Yesu kwa wenye dhambi! Aliteseka hivi vyote ili kuwaokoa wenye dhambi.

NI NINI KILICHOLETA TOFAUTI?

Miaka mitano iliyopita watu wawili waliishi katika nchi hii. Wote sasa wamekufa. Mmoja yuko mbinguni na mwingine yuko jehanamu. Ni nini kilichokuwa tofauti kati yao? Tofauti ilikuwa kwamba mmoja wao aliongozwa kuona kwamba yeye ni mwenye dhambi na Yesu alitolewa kwake kama mwokozi wake, na hapo baadaye akaishi maisha matakatifu. Alipokufa alienda mbinguni.

Yule mtu mwingine aliamua kwamba wakati mmoja atamkubali Yesu kama mwokozi lakini akaweka mbali uamuzi huo. Wakati huo alikuwa amemkataa mwokozi wa pekee. Mungu alimaliza maisha yake katika dhambi zake na sasa yumo jehanamu akighahiri wazimu wa kuumkataa mwokozi mkuu namna hii. "Ungali una wakati wakutosha" huu ndio uwongo mkuu wa shetani.

DHAMBI NI NINI?

Hebu tuangalie dhambi kutoka kwa mwangaza wa Biblia; kulingana na utakatifu wa Mungu. Isaya alipoona utakatifu wa Mungu alisema "Ole wangu kwa maana nimepotea kwa sababu mimi ni mtu mwenye midomo michafu na macho yangu yamemwona mfalme, Bwana wa majeshi". Mungu ni Mungu wa upendo, lakini upendo wake ni wa Mungu mtakatifu. Ametuambia kuhusu njia ya kupitia kwa kristo jinsi awezavyo kumsamehe mwenye dhambi aliyekosa kabisa. Lakini hawezi kusamehe isipokuwa kupitia kwa Kristo.

Tazama dhambi katika mwangaza wa hukumu ya Mungu. Pitia katika Biblia na uone ni kiasi kipi Mungu anachukia dhambi.

Malaika walioanguka katika dhambi, aliwatupa kutoka mbinguni, kwa maana anachukia dhambi. Alimfukuza Adamu na Hawa kutoka shambani mwa Edeni kwa maana anaichukia dhambi. Aliuweka ulimwengu wote chini ya mafuriko, hadi kila roho ikazama, kwa maana anaichukia dhambi. Na ulimwengu huu, ambao umechafuliwa sana na dhambi, utachomwa na moto mkuu siku moja. Kwa nini? Kwa sababu Mungu huchukia dhambi.

Tazama dhambi katika mwangaza wa Hukumu ya milele. Katika Mathayo 25 Yesu alisema kuhusu kundi kubwa la watu: "Hawa wataenda katika hukumu ya milele" Katika Biblia neno sawa linatumiwa Kueleza hukumu ya milele ya waliopotelea jehanamu, na raha isiyo na kikomo ya watu wa Mungu mbinguni, iwapo moja sio ya milele na ile nyingine sio.

ITAKUWA MUDA UPI?

Umewahi kuwaza uzima wa milele? Mwandishi mmoja maarufu alisema "Pengine mdudu mdogo angechukua dunia hii kwa meno yake madogo kupeleka katika nyota ya mbali. Mamia ya milioni ya miaka ingehitajika kwa kukamilisha safari moja. Mdudu ataanza kwa tawi la mti, na kuuchukua mzigo wake mdogo, na kisha kuianza safari ambayo pengine haina mwisho. Baada ya mamilioni ya mamilioni ya miaka kupita, afika tena kwa mzigo wake wa pili, Oh ni muda upi utapita kabla tawi moja halijaondolewa! Ni kiasi kipi wakati ujao ambao mti mzima utakuwa umekwisha. Msitu mzima utakwenda lini. Na ni lini yule mdudu atarudi tena kuichukua chembe ya mwisho ya sayari hii na kuibeba katika safari hiyo ndefu kabisa? Hata hivyo, milele ingekuwa ndiyo imeanza" Hukumu ya milele ni nini? Ni dhihirisho la chukizo la Mungu kwa dhambi

TAZAMA MWANA KONDOO WA MUNGU

Tazama dhambi katika mwangaza wa kifo cha Kristo kama ondoleo la dhambi. Ikiwa kitu kilipungua, au kitu kinginecho, isipokuwa kifo cha Kristo kingeweza kuondoa dhambi Mungu angalimhifadhi mwanawe wa pekee. Mfikirie akiipaza sauti yake angani na kilio

chake na kulowesha donge la udongo na majani yake kwa jasho lililokuwa na damu, na hata alipolia mara tatu "Ee Baba yangu, ikiwa ndiyo mapenzi yako niondolee kikombe hiki mbele yangu sio mapenzi yangu mbali mapenzi yako yafanyike." Ni uchungu ulioje Yesu alioubeba, wakati-yeye aliyekuwa amepewa nguvu na Mungu kuvumilia - alilia hivyo.

Kungekuwa na uwezekano kikombe hiki kimwondokee hivyo sisi,masikini wenye dhambi, tungeokolewa kisipokuwepo, kilio chake kingesikika. Lakini haikuwezekana. Mungu lazima aonyeshe kutopendezwa kwake na dhambi, hata kama zikibebwa na mwanawe. Kwa hivyo aliuficha uso wake kutoka kwake mpaka akalia "Mungu wangu, Mungu wangu, mbona umeniacha?"

Tazama dhambi katika mwangaza wa wema wa Mungu na upendo wa Mungu kwako. Ukimpiga adui ni dhambi. Ukimpiga rafiki ni dhambi kubwa. Lakini ukiinua mkono wako na kumpiga babako mpenzi, ni dhambi kiasi kikubwa pia, ni dhambi Kiasi gani basi lazima iwe, kwako wewe kupigana na Mungu mzuri kama alivyo Bwana?. Je hajakumiminia na fadhili zake na huruma zake tangu ulipozaliwa?

YESU ABISHA MLANGO WA MOYO WAKO

Vile Yesu amebisha mlango wa moyo wako, akingojea kuingia ndani na kuyabeba makosa yako, na kukaa ndani yako na Roho yake, na kukufanya mtakatifu! Amebisha kupitia kwa maombi ya mama yako. Amebisha kupitia kwa maagizo ya mwalimu wako. Alibisha wakati ule ulikaza moyo. Alibisha tena na tena kwa mahubiri ya injili. Alibisha wakati baadhi ya marafikize walipookolewa. Alibisha ulipokuwa mgonjwa. Ni ubaya kiasi kipi dhambi zako zimekuwa kwake Mungu mzuri kiasi hicho, ambaye amekupa nafasi kama hizo.

Hasa tazama dhambi katika mwangaza kwani kipi kinachonuiwa kwako kwa kumkataa Kristo. Dhambi kuu kuliko zote - dhambi ya kuhuzunisha - ni kwamba hutakikuja kwa Kristo. Mungu alimtuma mwanawe kuja kukutafuta na kukuokoa. Ametosheka kabisa na kifo cha Kristo kwa wenye dhambi, ya kwamba inamfurahisha

kuwasamehe wenye dhambi kwa ajili ya Kristo. Na mpaka kufikia wakati huu umemkataa mwanawe. Oh kwamba ungeona dhambi ya kumkataa Kristo, ya kuikanyagia chini damu yake, ya kukimbilia jehanamu juu ya mwili wake uliokufa - na kusema: "Hasha mimi sitakuhitaji kama mwokozi wangu."

"Mtu asipozaliwa mara ya pili hawezi kuuona ufalme wa Mungu" Ndivyo Yesu alimwambia Nikodemu mara tatu jioni moja. Msomaji - wewe umezaliwa mara ya pili? Umewahi kupokea mabandiliko ambayo yangeitwa kuzaliwa upya? Katika kitendo cha kuja kwa Kristo unazaliwa mara ya pili. "Bali wote waliompokea aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu" Yohana 1:12

ROHO AMBAYO IMEPOTEA

Biblia inasema "Mshahara wa dhambi ni mauti" na kila roho itendayo dhambi itakufa". Mauti inayozungumziwa hapa inahusisha yale yote Mungu anampiga mwenye dhambi aliyepotea kama majuto ya dhambi.

Kila mwenye dhambi "tayari ameshahukumiwa," ingawa anaishi" Yohana 3:18. U kama mtu aliyehukumiwa kifo kwa kuua, ukilala gerezani ukingojea wakati wa kuuawa. Mtumishi wa Mungu, kifo chaweza kuja haraka kukuita.

Gadhabu ya Mungu inakukalia. Yohana 3:36. Mungu anakasirishwa na waovu kila siku.

Wewe u mtoto wa ibilisi na u mtumwa wake. Ibilisi ndiye adui mkubwa wa Mungu na mwanadamu. Hupenda kuharibu mwili wako na roho yako. Yeye ndiye bwana wako. Unafanya siku kwa siku yale ambayo ibilisi angependa ufanye. Na kati ya mabwana wote yeye ndiye mkatili zaidi.

Utakufa siku moja, na huenda ikawa hivi karibuni na kwa ghafula. Na ni nini hufanyika katika kifo? Mapepo hukizunguka kitanda cha kifo cha mwenye dhambi, na mara afapo, kumchukia na kumpeleka kwa shimo lisilokuwa na mwisho.

Siku itafika utakapoisikia tarumbeta ya Mungu, na utainuka kutoka ndani ya kaburi lako. Ikiwa ulikufa bila Kristo roho yako iliyoharibika italazimika kuingia katika mwili wako ulioharibika, na sharti utasimama mbele ya Bwana katika hukumu.

Kitabu cha Mungu kitafunguliwa. Kila neno mbaya ulilolisema na kila tendo mbaya ulilotenda litasomwa mbele ya walimwengu walio kusanyika. Na utaisikia sauti ya Yesu ikisema "Ondoka kwangu wewe uliyelaaniwa, katika moto wa milele uliotayarishiwa ibilisi na malaika wake."

NA ITAKUWA YA MILELE

"Hawa wataenda katika hukumu ya milele." Ndiyo wewe "utaenda" mbali na baba na mama yako utakuwa mbali na nyumbani kwako, sabato zako, mikutano yako, -mbali-katika hukumu ya milele.

Hebu tuwaze kuhusu minyoo itakayo kutafuna katika mahali pa taabu. Mnyoo mmoja utakuwa ni tamaa zako ambazo hazitatoshekea jehenamu. Mnyoo mwingine utakuwa mawazo yako. Utakumbuka nyakati zile haukuwa mbali na ufalme wa Mungu na sasa umepotea milele. Mnyoo mwingine utakuwa marafiki zako katika taabu, viumbe wabaya wakuchukiza. Humo utawakuta watu uliowaongoza katika dhambi, na watakulaani milele.

Na itakuwa milele. Huu ndio uchungu wa laana. Biblia inasema: "Moshi wa taabu zao utapaa juu milele na milele." Ikiwa baada ya mabilioni ya miaka kungekuwa na mawazo ya kuwa huru, kungekuwa na tumaini jehanamu. Lakini hayatakuwako. Hakuna matumaini jehanamu Oh milele! milele! Umeshawahi kuwaza kuwa jehanamu wakati wote wa milele isiyo na mwisho?

NA NINI BAADAYE?

Siku moja katika chuo kikuu, kijana mmoja alikuwa akimweleza mkufunzi kuhusu mipango yake ya siku zijazo. Alimwambia ataenda kusoma awe wakili. "Nini baadaye?" "Kisha nitasomea digrii yangu ya udaktari." "Nini baadaye?" "Kisha nitaziweza baadhi ya kesi

ngumu ngumu, na nitapata sifa kubwa" "Nini baadaye?" "Halafu nitapandishwa cheo katika baadhi ya ofisi kuu, na niwe tajiri."Na ni nini baadaye?" "Nitaishi na mali na heshima" "Nini baadaye?" akauliza mkufunzi "Na halafu - na halafu - nitakufa." Hapo yule mkufunzi akaipaza sauti yake na kuuliza kwa sauti kubwa. "Na nini baadaye?" Yule kijana hakufanya jawabu, aliinamisha kichwa chake na kuenda zake. Kisha baadaye aliji toa kwa Kristo, na kuishi maisha matakatifu na ya manufaa.

BARAKA 14 NDANI YA KRISTO

Ningependa ujue kile unachopata unapompokea Kristo kama mwokozi wako. Sio kile unachopata baada ya miaka mingi; lakini kile unachopata kwa haraka kama umeme, kwa wakati ule ule, unapo kuwa na imani mwamini Yesu kuwa mwokozi wako. Unapata hizi kwanza nazo na kukubeba katika safari yako mbinguni.

1. Unapata msamaha wote na wa bure wa dhambi zako. Soma Matendo ya mitume 13:38,39" Basi na ijulikane kwenu, ndugu zangu, ya kuwa kwa huyo mnahubiriwa msamaha wa dhambi, kwa yeye kila kuhesabiwa haki kwa torati ya Musa "Kwa yeye" kwa Kristo. "kila aaminiye - sio tu wengine" "huhesabiwa haki" hii inamaanisha wamesamehewa bure.

2. Dhambi zako zinaondolewa kutoka kwako. Mungu asema kwamba dhambi zako zimetupwa nyuma ya mgongo wake. Hazioni. Isa. 38:17. Asema tena: "kama vile mashariki ilivyo mbali na magharibi ndivyo alivyotoa dhambi zetu mbali nasi. Zaburi 103:12. Ni umbali gani mashariki ulioko mbali na magharibi? Anaendelea kusema: "Dhambi zao na uasi wao sitaukumbuka tena kabisa." Waebrania 10:17. Dhambi sio tu kusamehewa bali pia kusahauliwa. Mungu asema ya kwamba umetakaswa "mweupe kuliko theluji". Zaburi 51:7.

3. Umeletwa katika wema wa Mungu. Hasira yake imegeuzwa kutoka kwako na "umekubaliwa katika huyo mpendwa." Waefeso 1:6.

4. Dhambi zako zote zimewekwa juu ya Kristo na wema wake wote juu yako na "umepata kuwa haki ya Mungu katika yeye."2 Wakorintho 8:21.

5. Unafanyika kuwa mwana wa Mungu-unapata, Mungu kuwa baba yako. "Bali wote waliompokea aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu, ndio wale waliaminio jina lake." Yohana 1:12.

TUMEITWA KUWA WANA WA MUNGU

6. Mungu anakupenda na anapendezwa kukuongoza na kukutunza, na kukutosheleza. Yesu aliomba "ili ulimwengu upate kujua mimi niko ndani yako nawe uko ndani yangu na kuwa wanipenda." Yohana 17:25. Tazameni ni upendo wa namna gani alilotupa Baba, kwamba tuitwe wana wa Mungu. 1 Yohana 3:1.

7. Unapata Roho mtakatifu wa Mungu kuishi ndani yako, na kukusaidia kuishi maisha matakatifu. Oh mwamini dhaifu, Mungu aishi ndani yako. "Hamjui ya kuwa ninyi ni hekalu la Mungu na Roho wa Mungu aishi ndani yenu. 1 wakorintho 3:16.

8. Unapata Roho mpya na hali mpya. "Nami nitawapa ninyi moyo mpya, nami nitatia roho mpya ndani yenu."Ezekieli 36:26. Atakuwezesha kujua mapenzi yake kuyapenda mapenzi na kuyafanya mapenzi yake.

9. Unapata toba na msamaha wa dhambi. Matendo 5:31. "Mtu huyo Mungu amemtukuza kwa mkono wake wa kuume, awe Mkuu na mwokozi,awape waisraeli toba na msamaha wa dhambi."

10. Unapata nguvu za kumpenda Kristo. "Sasa twapenda kwa maana yeye alitupenda sisi kwanza." 1 Yohana 4:19. Upendo huzaa upendo. Unapozidi kuuona upendo wake kwako, ndivyo utakavyompenda zaidi.

11. Utapata nguvu za kuomba katika jina la Yesu. Wema wake unawekwa juu yako, na unaweza kuja kwa Mungu katika jina lake, kuitisha timilizo la ahadi zake.

12. Unapata nguvu za kutenda kazi nzuri, na kumpendeza Mungu. Jambo la kwanza unalofanya kumpendeza Mungu, ni wakati ule unapo mpokea Kristo kama mwokozi wako. Baada ya hayo kazi yako na huduma zitampendeza yeye.

13. Unapata ahadi za kupendeza kutoka kwa Biblia kama zako. ‘“Maana ahadi zote za Mungu zilizopo katika yeye ni ndiyo; tena kwa hiyo katika yeye ni Amini Mungu apate kutukuzwa kwa sisi”.2 Wakorintho 1:20. Ni utajiri ulioje katika hizi ahadi.

14. Unapata uzima wa milele, Yesu alisema “Amin, Amin nawaambia, yeye aniaminiaye yuna uzima wa milele.” Yohana 6:47. Unapata mbinguni kuwa mji wako, Yesu alisema “Nyumbani mwa Baba yangu mna makao mengi; kama sivyo ningaliwaambia, maana ninaenda kuwaandalia mahali. Basi mimi nikienda na kuwaandalia mahali nitakuja tena niwakaribishe kwangu, ili nilipo mimi nanyi mwepo.” Yohana 14:2-3.

Hizi zote ni baraka unazipata wakati ule unapotumaini Kristo kama mwokozi wako. Paulo anazungumzia kuhusu “utajiri usioweza kueleweka ndani ya Kristo.” Ni utajiri wa rangi na manukato, na urembo umefichwa ndani ya waridi chipukizi kwa wakati wake! Na utajiri usiovumbulika ndani ya Kristo!

“Bwana pasipo wewe, sisi tu masikini, twaa tulicho nacho; na tukiwa nawe tu matajiri, twaa unachopenda.”

WOKOVU BURE KWA WOTE

Wakati safina ya Nuhu ilipomalizika, yeye na Jamaa yake iliwabidi waingie ndani ya safina, ama waangamie katika mafuriko. Ilikuwa ni hatua lakini ilibidi ichukuliwe.

Wakati yule malaika mharibifu alipopita juu ya Misri, aliupita kila mlango ambapo damu ilinyunyizwa. Kwa hivyo damu ya Kristo

lazima inyunyizwe kwa moyo wako.

Kama vile sadaka ya kuteketezwa ilivyotolewa kama ondoleo la dhambi nasi lazima tuzikiri dhambi zetu waziwazi kwa Mungu, na kuziweka juu ya Yesu;la sio hivyo hatuwezi kuokolewa. Unawezaje kupata kifo cha Yesu kama ondoleo la dhambi zako? Ni kwa kukichukua kwa imani tu. Ni kwa kizitegemea ahadi za Yesu. Yesu anatoa kifo chake kwako, kwa wakati huu, kama ondoleo la dhambi zako zote.

Kuukubali mwito wa msamaha inamaanisha kukiri dhambi zako kwake, na kusema "Bwana Yesu, wewe unakitoa kifo chako kuondoa dhambi zangu. Hapa na sasa ninakubali mwito wako. Ninachukua kifo chako kama ondoleo la dhambi zangu, na ninakuchukua kama mwokozi wangu."

Siku moja mtu masikini na dhaifu alikuwa akitembea njiani akibeba mzigo mzito. Akiendelea mtu mmoja mwenye nguvu akaja na kumwambia "Huo mzigo wako ni mzito sana kwako; nipe nami nitakubebea, na nitakupumzisha." Kisha yule mtu masikini dhaifu akamkabidhi ule mzigo kwa yule mtu mwenye nguvu. Na vivyo nilikuwa nimebeba mzigo wangu wa dhambi na Yesu akaja akisema "Utwike mzigo wako Bwana, naye atakuhifadhi" na nikampa mzigo wangu wa dhambi kwake naye amechukua.

Ukiwa utamtafuta kwa imani haba, punde utasema ukifurahi, "Nimempa yeye yule roho yangu imependaye." Soma ahadi katika 2 Wakorintho 5:20,21. "Yesu alifanywa dhambi kwa ajili yetu - tumefanywa haki ya Mungu ndani yake- Mungu atusihi tuunganishwe naye - Yesu anatombea - ni ahadi zilizoje kukuhimiza upokee kwa imani karama ya Mungu ambayo ni uzima wa milele kupitia kwa Yesu Kristo Bwana wetu."

WOGA USIO NA MSINGI

Unaweza kujaribiwa kufikiria "Dhambi zangu ni kubwa sana kusamehewa." lakini wewe fikiria mateso ya Kristo, na huamimi vile Mungu asemavyo; "Damu ya Yesu Kristo, mwana wake,

hututakasa na dhambi zote".

Fikiria kuhusu 1 Wakorintho 6:9,10 "Au hamjui ya kuwa wadhalimu hawatauridhi ufalme wa Mungu? Msidanganyike waasherati hawatauridhi ufalme wa Mungu, wala waabudu sanamu, wala wazinzi, wala watamanio, wala wezi, wala watukanaji, wala wanyang'anyi". Ni orodha nyeusi aje!

Lakini usisimame pale. Endelea na kusoma: "Na baadhi yenu mlikuwa watu wa namna hii, lakini mlioshwa, lakini mlitakaswa, lakini mlihesabiwa haki katika jina la Bwana Yesu Kristo, na katika roho wa Mungu wetu". Mistari hii ikiwa katika Biblia usife moyo juu ya wokovu wako, au wokovu wa mtu yeyote aliye hai. Usifikirie tena wewe u nani, lakini fikiri jinsi Yesu alivyo mwokozi wa ajabu.

WAKATI WA KUTUMAINI

Sio kitambo sana nilikuwa nikitembea na kijana mmoja. Nilimwuliza jinsi alivyoongozwa kwa Kristo na akaniambia: "Binamu yangu aliniandikia akaniuliza niende kuwatambelea nyumbani na nikaenda. Binamu yangu hakunizungumzia moja kwa moja kuihusu roho yangu, lakini alinieleza vile mwanamke mwingine alivyoletwa kwa Kristo. Tom, aliniambia, huyu mwanamke mchanga alikuwa na hamu ya kuokolewa, lakini aligundua kwamba hawezi kujiokoa kwa yale yote aliyotenda na bidii yake.

Kisha akaona Yesu aliumizwa kwa ajili ya maovu yake na alijeruhiwa kwa makosa yake, na kwamba alizitwaa dhambi zake katika mwili wake mtini. Aliona kwamba anahitaji kupokea adhabu ya dhambi zake, ikiwa hatakubali kumpa Bwana kuitwaa yote Yesu alimaliza hiyo kazi.

Aligundua ya kwamba alihitajika kuomba tu, Asante Ee Bwana Yesu, ninachukua kifo chako kuondoa dhambi zangu, na ninakuchukua kuwa mwokozi. Alipumzika ndani ya Kristo na kifo chake kwa msamaha, na ungeweza kuona jinsi alivyofurahi ndani ya Yesu.

Kisha akasema sasa Tom ungependa kujua kwamba dhambi zako zimesamehewa? Nilikuwa na uhakika kwamba nilitaka kuokolewa. Tulipiga magoti na akaomba. Mara niliamini ya kwamba nilikuwa nikipumzika katika Kristo, na nikasikia kana kwamba nashawishiwa kusimama kutoka magotini na kusema, Ninaamini! Ninaamini! lakini ibilisi ni kama alininong'onezea,"usijifanye mjinga - ni uwongo mtupu - hisia tupu - furaha ipitayo".

Kisha roho wa Mungu akaanza kufanya kazi ndani ya moyo wangu tena na kuwaonyesha kwamba Kristo alitaka kuchukua dhambi zangu na kuniokoa. Niliruka kwa miguu yangu na kusema, Ninaamini! Ninaamini! Binamu yangu akasimama pia, na kufurahi pamoja nami ndani ya mwokozi.

Halafu akaanza kuniambia mbinu za ibilisi na vile atajaribu kunidanganya. Tom, alisema, kesho asubuhi, ibilisi atakuwa na uhakika kukwambia kwamba yote yalikuwa ni uongo. Hakuna kitu kama kifungu cha maandiko unapopigana na ibilisi. Mwambie Kristo, yeye mwenyewe, alizibeba dhambi zetu mwilini mwake mtini (1 Petro 2:24), au yeye anijiaye kamwe sitamtupa nje (Yohana 6:37). Mwambie anamtengemea Kristo na utamtengemea Kristo".

Tena alisema kwamba ibilisi ana uhakika wa kuleta mawazo mabaya akilini mwangu, na kisha kuniambia kwamba ni mbaya kama awali. Akaniambia pia, ya kwamba ibilisi ataniambia kwamba kwa hakika nitaanguka. Nami ningelimwambia kwamba ni ukweli siwezi kusimama peke yangu lakini mwokozi wangu Yesu aliahidi ataniweka nisianguke.(Yuda 24), na kwamba "jina lake ataitwa Yesu maana ndiye atakayewaokoa watu wake na dhambi zao." (mathayo 1:21).

Baadaye nikamwambia ndugu yangu yote niliyofunzwa ya Yesu, na ilikuwa ni wakati mrefu kabla hajabadilishwa, na tumekuwa wa faraja kubwa kwa kila mmoja,tangu siku hiyo. Dada yangu mdogo, ambaye sasa amekufa, naye aliyeletwa kwa Kristo pia.

Sasa, msomaji wangu mpenzi, unaona Mungu ametosheka na kifo cha Kristo msalabani kwa ajili ya mwenye dhambi, kwamba anataka kukusamehe sasa kwa ajili ya Kristo. Hauhitajiki kufanya

jambo kuondoa dhambi zako, ikiwa unataka kumkubali Kristo. Kristo sasa yuko kando yako, akikuomba umruhusu azichukue dhambi zako na kukubebea.

Oh, fanya vile akuhimizavyo - "Njooni kwangu, nyote mlemewao na mizigo mizito, nami nitawapumzisha." Mathayo 11:28. Njoo kwake leo.

BIBLIA

Kitabu hiki kinayo - mawazo ya Mungu, hali ya mwanadamu, njia ya wokovu, mwisho wa wenye dhambi na furaha ya waamini.

Mafundisho yake ni matakatifu, kanuni zake kweli, visa vyake ni vya ukweli na maamuzi yake hayabadiliki. Kisome uwe na busara, kiamini uwe mafichoni, na kipende uwe mtakatifu.

Kinao mwangaza wa kukuongoza, chakula cha kukusaidia, na faraja ya kukuchangamsha. Ndiyo ramani ya msafiri, fimbo ya mpita njia, dira ya rubani, upanga wa askari na maktaba ya mkristo.

UTAKATIFU KWA IMANI NPANI YA KRISTO

Utakaso ni kazi ya Roho wa Mungu aishipo rohoni. Lakini Roho wa Mungu afanya hivi aje? Kwa kugeuza jicho la mwamini kumwelekea mwokozi mpendwa aishiye. Katika mwisho wa Warumi, kifungu cha saba Paulo auliza: "Ni nani atakaye niokoa na mwili huu wa mauti?" Kisha panakuja Jibu: "Ninamshukuru Mungu ndani ya Yesu Kristo Bwana wetu."

Unakumbuka jinsi ulivyobadilishwa. Ilikuwa kazi ya Roho wa Mungu; alilibadilisha jicho lake kumwelekea Yesu akifa msalabani kwa ajili ya wenye dhambi na akakuonyesha alivyotamani kukuokoa. Na wakati ule ulipookolewa ulikuwa ukifikiri juu ya Kristo.

Na kama vile roho wa Mungu hutakasa, huyangeuza macho yetu kwa Yesu. Paulo hakuuliza ni nini kitakachoniokoa. Hakuna kile kinachoweza kutuokoa, lakini kunaye - Mwokozi mpendwa aishiye ambaye aweza, "Ninamshukuru Mungu ndani ya Yesu Kristo Bwana wetu."

Ukweli huo unafundishwa katika 1 Wakorintho 1:30. Sisi tu ndani ya Kristo na Kristo yu ndani yetu. Hatuna busara lakini Kristo ndiye busara yetu. Hatuna haki lakini haki ya Kristo ni ya bure kwetu kama mwangaza wa jua. Hatuna chanzo cha utakatifu ndani yetu, lakini Kristo ndiye utakaso wetu na ukombozi wetu.

Wakati ule ulipowezeshwa umkubali Kristo, ulifanywa mmoja na Kristo. Kristo alikufa, nawe ndani yake. Kristo aishi nawe ndani yake, Jihesabu kuwa umekufa katika dhambi, na umefufuliwa pamoja na Kristo. Jivishe Kristo. Mwache aishi ndani yako. Kula naye. Mpende. Kaa ndani yake, na dhambi itaanguka kutoka kwako. Moyo ulio na Kristo umeshatolewa utumwani: uko Huru.

YESU NDIYE MZABIBU WA KWELI

Kristo ndiye mzabibu wa kweli na wewe ni tawi. Yohana 15. Hupendeza mzabibu kulipa tawi uhai na nguvu. Tawi halikui na kuzaa tunda kwa kutumia bidii nyingi au kwa kuzozana. Hukaa tu ndani ya mzabibu, na kupata nguvu na kunawiri kutoka kwa mizizi. Ndivyo Kristo hupendezwa kutupa sisi - matawi yake - neema na nguvu kila wakati.

Yesu yuko hapa, na amenunua utimilifu wote wa Roho yake kwa kila mmoja wetu. Humpendeza yeye kutujaza kila wakati. Anatuamrisha "Tujazwe na Roho", na anataka kutujaza sasa. je hatutaamini, Tukihisi au tusipohisi ya kwamba atujaza. Ikiwa tutatatenda hivyo, haitakuwa muda mrefu kabla Mungu hajatupa maarifa mbali zaidi na yale tunayoyafurahia sasa.

Hapa tunakuja kwa kutumia mbinu. Hatutawekwa tukimtegemea Kristo siku kwa siku, na saa kwa saa, isipokuwa tutumie njia ya neema. Tunastahili tujishikamanishe na kanisa la imani ya injili ambapo injili inahubiriwa, tunastahili kuhudhuria ibada zake, na kuhusika katika kazi za kikristo. Tunastahili kwenda kwenye meza ya Bwana kiasi tupatapo nafasi. Hatustahili kwenda mahali penye majaribu, au kufanya urafiki na wale ambao ushirika wao utatudhuru.

Na ni lazima tuzisome Biblia zetu pamoja na maombi. Goerge Muller, katika kila hotuba anazopeana, hujaribu kuwahimiza wasikilizaji wake kuhusu umuhimu mkubwa wa kuisoma Biblia pamoja na maombi. Kwa kweli hatuwezi kukua katika neema pasipo hili. Basi hii ndiyo siri ya utakatifu - mtazamo wa maisha marefu ya Yesu Kristo.

JINSI YA KUWA NA UHAKIKA

Hakikisho la wokovu ni kazi ya Roho wa Mungu. "Roho mwenyewe hushuhudia pamoja na roho zetu, kuwa sisi tu watoto wa Mungu" Warumi 8:16, jinsi ya kupata hakikisho ni kumtazama Yesu - na kuja kwake - kama alivyofunuliwa katika Biblia.

Duncan Matheson alisema: "Niliwezeshwa kumchukua Mungu kwa neno lake. Sikumwona mwingine ila Yesu peke yake, na yote katika kazi ya ukombozi. Mzigo wangu ukaanguka kutoka mgongoni mwangu, na nikaokolewa. Sikuweza kujizuia kwa furaha, niliimba wimbo mpya, wokovu kupitia kwa damu ya mwana-kondoo. Nilisikia utulivu wa mwenye dhambi aliyesamehewa. Nilimwona mtu Yesu pekee, nililia kwa dhambi zangu zilizomtundika msalabani, na yalikuwa machozi ya toba ya kweli."

"Ni wake milele wake pekee;
Ni nani mimi na Bwana kututenganisha?
Oh na pumziko lenye raha ya aina gani
Kristo anaweza kujaza roho inayoipenda!"

MBINGUNI - NYUMBANI KWETU

MWINJILIST. W. P. NICHOLSON

Yesu alisema, "Nyumbani mwa Baba yangu mna makao mengi, kama sivyo ningaliwaambia; maana naenda kuwaandalia mahali" Yohana 14:2. Hakuna somo lingine ambalo huiyeyusha roho na kuyawasha mawazo kuliko zaidi kuliko somo la mbinguni. Je tumechoka na vita na mizozo ya maisha? Sio busara kujua kwamba karibuni tutakuwa mbinguni ambapo hakutakuwa na vita vingine au mizozo mingine, na ambapo hatuchoki tena.

Mbinguni ni mahali pa kung'aa. Hakutakuwa usiku huko. Ni siku moja ndefu ya milele. Bwana ndiye taa ya mbinguni. Nchi hiyo ing'aayo haijaweza kuzimwa na huzuni. Wamevaa mavazi meupe huko juu - uchungu haujulikani huko, hakuna aukwepaye. Wengi wana uchungu mwingine moyoni kuliko uchungu wo wote mwilini - mtoto kutoweka katika dhambi. Mtu ye yote anaweza kufafanua uchungu anaoupitia mama kama huyo.

Halafu mbinguni kunang'aa kiasi kwamba hakuna jicho litazimia kwa machozi. Hakuna laana pale. Ni wangapi wamelaaniwa na dhambi hapa. Mshukuru Mungu! tunaenda kwa ulimwengu ambapo laana na kupoozesha kwa dhambi milele hakumo. Mbinguni pia ni pahali ambapo ni pa furaha. Tunasoma kuhusu waimbaji wakiimba na uimbaji uliokombolewa "kwake yeye aliyetupenda na kutufungua kutoka kwa dhambi zetu na damu yake."

WATOTO WA MBINGUNI

Dr. Guthurie wa Edinburgh, asema, "Mbinguni inakusanyika hasa watoto wadogo." Kwa maana ufalme wa mbinguni ni wao; ni kiasi kipi maneno haya yatuliza kutoka kitandani mwa mtoto mchanga anayekufa.

Yanaanguka kama matone ya dawa juu ya roho zitokazo damu, tunapotazama kudhoofika hayo maisha machanga, hadi, na kupumua taratibu, mtoto wetu mchanga anapotoka mwilini, na kupaa kwenda

kwa sifa za uzuri wa mbinguni, na kifuani mwa Mungu wake."

Mbinguni ni pahali pa ufahamu wa nafsini. Hapa twajuana visivyo vikamilifu. Tutajuana vyema wakati ukungu utaondolewa. Petro alimtambua Musa na Eliya katika mlima wa mageuzi. Wakati malkia Victoria mzuri alipokuwa akifa, alisikika akisema "Albert, Albert." Mume wake aliyekufa miaka mingi mbeleni, alikuwa karibu naye. Mwanamke mmoja aliniambia wakati mtoto wake mdogo alikuwa akiaga, alilia, "Baba, Baba." Baba yake alikuwa ametangulia wakati uliopita.

YERUSALEMU MPYA - MJI WA MBINGUNI

Ni mji wa aina gani huo utakaokuweko. Hakuna vijiji au magari madogo madogo huko. Hakuna hospitali au jela. Hakuna masikini au wanaonyanyaswa. Mambo yale yanayoilaani miji yetu mikubwa mikubwa hapa, hayatakuweko mbinguni. Mji ambao Mungu ameuandaa sio wa kuharibika kwa wao wakaao ndani yake, hata kwa vitu vyake. Lulu yake, na yaspi yake na dhahabu yake safi, sio vya kuharibika ili kudumu katika vitu visivyoharibika. Hakuna kilio cha kifo kipo katika makazi ye yote yake. Hakuna mazishi yanayozitia giza njia zake. Hakuna mifano ya sanamu takatifu yang'aa katika vilima vyake vya milele.

Mitaa ya mji mtakatifu ni ya dhahabu safi. Makao yake ni majumba. Wakaazi wake ni watakatifu na wenye furaha. Haujajengwa kwa mikono, hawatazimia kwa urefu wa miaka ya wakati. Ni mji ambao wakazi wake hawana hesabu ya watu waliohesabiwa; na kupitia mitaa yake, hakuna mkondo wa biashara unaendelea. Ni mji bila ya makaburi au msiba, bila dhambi au huzuni, bila kuzaliwa au kuzikwa, bila ndoa au matanga. Ni mji ung'aao kwa kuwa na Yesu kama mfalme wake, malaika kama walinzi wake, wateule kama wenyeji wake; na ambazo kuta zake ni wokovu, na milango yake ni sifa.

GEREZA YA MUNGU

Katika nchi hii yetu iliyostaarabika tunazo gereza kubwa. Ni aibu gani kuwatupa wanaume na wanawake mahali kama hapo pa kuteseka, kuwaibia uhuru wao na nafasi zao; kuwatenganisha wanaume kutoka kwa nyumba zao na jamii zao. Wakati mwingine watu wako jela kwa sababu wame fanya makosa kosa na baadhi ya wengine tunawanyonga.

Tuna wakimbizi wengi kote katika nchi. Maelfu ya watu wamewekwa pale kinyume cha mapenzi yao. Sio aibu kuwa na mahali kama hapo, na kuwatendea watu hivyo?. Ungeniangalia kwa huzuni kama ningezungumza nawe hivi, na kustaajabu nimetoka wapi. Ungesema "Hujui kuwa watu hawa ni wavunja sheria na wazimu? Ni kwa ajili ya wema wao na usalama wa nchi na watu tunawaweka huko".

Unafikiri tunazo hisia nyingi kuliko Mungu? Ni kina nani wanaenda jehanamu? Ni wanaume na wanawake waliomwasi Mungu na kukataa kuokolewa na damu ya mwanawe. Ni kipi kingine Mungu angewafanyia isipokuwa kuwatupa gerezani. Kwa kweli mtu wazimu huipoteza roho yake binafsi kwa kumkataa Yesu Kristo kama mwokozi wake, wanaume na wanawake jehanamu ndiyo gereza ya Mungu; Jehenamu ni mahali pa wakimbizi.

Ukiendelea kumwasi Mungu - Mungu ana jela kwa ajili yako, na ikiwa wewe ni mjinga sana kukataa wokovu wake, Mungu ana kimbilio kwako.

Acha nikupe baadhi ya maneno hutumiwa na Mungu kueleza hali ya mahali hapa: "Ziwa la moto" - shimo lisilo na mwisho lenye moto wa kuharibu - mahali pa huzuni - ambapo watalia - mahali pa kilio - tanuru - mahali pa mateso - kuchomeka kwa milele - mahali pa chafu - mahali wanapo mlaani Mungu - uharibifu wa milele - mahali pa giza ya nje - ambapo hapana pumziko - adhabu ya milele - ambapo watatafuna ndimi zao - mahali palipotengenezewa shetani na malaika zake - ambapo wanalilia tone la maji - wakiteswa na moto na kiberiti - moto wa jehenamu - ghadhabu ijayo.

Ikiwa Mungu hakuwa na upendo angalitengeneza njia ya jehenamu rahisi na ya haraka, lakini ameilinda njia hiyo ina miiba na vizuizi, na mtu lazima afanye bidii kufikia pale. Lazima azichome hisia tena na tena. Lazima ajikwae juu ya machozi na maombi ya watu wa Mungu. Lazima alinyamazishe neno la Mungu, kumzima Roho Mtakatifu, na kujikwaa mguu kwa damu ya dhabihu ya Kristo; haya yote kabla hajafaulu kuupoteza moyo wake milele.

JINSI YA KUFAULU KATIKA MAISHA YA KIKRISTO

NA DR. R. A. TORREY

Kunavyo vikundi viwili vya watu wanaoanza maisha ya kikristo; wale ambao wanaanguka kabisa au wale ambao waanguka kidogo na wale ambao wanafaulu kabisa. Swali kwa ghafula lakuwaza; Inawezekana kuonyesha njia dhahiri ambayo ye yote atakaye, anaweza kuitembea, na kuifuata aweza kuwa na uhakika kwamba atafaulu? Ninaamini iko. Ninaamini neno la Mungu lina mafundisho machache rahisi ambayo yakifuatwa yataleta uhakika wa kufaulu katika maisha ya kikristo. Kunazo hatua katika njia ambazo zimeonyeshwa katika Biblia.

1. ANZA VYEMA: Nini mwanzo mwema tunaona Yohana 1:12 “Bali wote waliompokea aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu,ndio wale waliaminio jina lake.” Mpokee Kristo. Mchukue kama mwokozi wako aliyekufa kwa ajili ya dhambi zako. Mtumainie jambo lote la kukusamehe. Tulia ndani ya Kristo kwamba amelipa deni yote ya dhambi zako.

2 Wakorintho 5:21 “Yeye asiyejua dhambi alimfanya kuwa dhambi kwa ajili yetu; ili sisi tupate kuwa haki ya Mungu katika yeye.” Wagalatia 3:13 “Kristo alitukomboa katika laana ya torati, kwa kuwa alifanywa laana kwa ajili yetu; maana imeandikwa, amelaaniwa kila mtu angikwaye juu ya mti.”

Ni katika hatua hiyo ya kwanza ambapo wengi hufanya kosa. Wanajaribu kuchanganya kazi zao nzuri kama nguzo ya wokovu. Wanafikiria kwamba ikiwa ni wazuri Mungu atawasamehea kwa sababu ya kifo cha Kristo na wema wao.

Mchukue kama mwokozi wako,yule atakaye kuokoa na nguvu za dhambi, yule atayekuhuisha utakapokuwa umekufa katika maovu na dhambi. Usijaribu kujiokoa na nguvu za dhambi. Mtumaini kuitenda.

MCHUKUE KAMA KIONGOZI WAKO: Usitafute kujiongoza maisha yako binafsi. Jisalimishe pasipo masharti kwa uongozi wake juu yako. Sema, "Yote kwa Yesu." Wengi hushindwa kwa sababu hurudi nyuma badala ya kujisalimisha kabisa. Wanataka kumtumikia Yesu na mioyo yao nusu, na sehemu yao wenyewe, na sehemu ya vitu vyao. Ni maisha maharibifu ya kujikwaa na kushindwa, maisha haya ya kujitoa moyo nusu. Ni maisha ya furaha njia yote, maisha ya kujitoa kabisa.

Ikiwa hujawahi kufanya hivyo na unatumaini "Kufaulu katika maisha ya Kikristo," enenda peke yako na Mungu, piga magoti na sema "Yote kwa Yesu" sema kwa kujitolea, sema kutoka ndani ya moyo wako. Kaa hapo hadi utambue inamaanisha nini na unafanya nini. Ni hatua ya ajabu mbele mtu anapoichukua. Ikiwa umeshaichukua, ichukue tena. Ichukue mara kwa mara. Kila wakati ina maana mpya na huleta baraka mpya.

Kumchukua Kristo kuwa mwokozi wako kunahusika kutii mapenzi yake, kiasi kile ukijuacho katika kila hali ndogo ya maisha. Hili ndilo jambo moja ya yale masharti muhimu ya kupokea "Roho mtakatifu ambaye Mungu amewapa wote wanao mtii". Matendo ya Mitume 5:32.

2. MKIRI KRISTO WAZI MBELE YA WATU. Mathayo 10:32 "Basi, kila mtu atakayemkiri mbele za watu, nami nitamkiri mbele ya Baba yangu aliye mbinguni." Warumi 10:10 "kwa maana kwa moyo mtu huamini hata kupata haki, na kwa kinywa hukiri kupata wokovu."

Maisha ya kukiri ni maisha ya wokovu kamili. Ni wakati tunapokiri Kristo mbele ya watu kwamba hutukiri mbele ya "Baba yangu aliye mbinguni," na utimilifu wa baraka zake huja.

Haimaanishi ya kwamba, tumkriri Kristo mara moja tu, kama kwa mfano, tunapoungana na kanisa, lakini kila mara. Yule awezaye kupata mafanikio makubwa ya maisha ya kikristo astahili kuitwaa kila nafasi ya kumkiri Kristo mbele ya watu - nyumbani, kanisani, sokoni, mahali pa kazi na kila mahali. Wakati mmoja nilimsikia mhubiri mmoja mzee mwenye hekima akisema, "Ukitengeneza maagano mema na Kristo, atafanya maagano makuu nasi." Ni wangapi walianguka kutoka kwa Kristo mahali hapa! Walienda katika mji mpya, au katika mahali papya pa kufanya kazi, na wakapuuza kumkiri Kristo, na sasa wamerudi katika dunia.

3. SOMA NENO: 1 Petro 2:2 "kama watoto wachanga waliozaliwa sasa yatamanini maziwa ya akili yasiyoghoshiwa, ili kwa hayo mpate kuukulia wokovu." Neno la Mungu ndicho chakula cha roho. Ndicho chakula cha maisha mapya. Yule apuuzaye neno hawezi kufaulu vyema katika maisha ya Kikristo. Wote waingiao katika maisha ya Kikristo ni walaji wakuu wa neno la Mungu. Wengi huanguka hapa. Mwulize aliyeteleza na kurudi nyuma "Umejilisha na neno kila siku?" Sijawahi kumpata mmoja aliyeweza kusema ameshawahi.

Mambo mawili katika kusoma biblia ni: kwanza, soma kwa chakula cha roho yako. Pili, soma kiasi kikubwa ukiwa katika magoti yako. Biblia imekuwa kwa njia ayingine kitabu kipya kwangu tangu nilipoanza kusoma hali ninapopiga magoti.

4. OMBA BILA KUKOMA: 1 Wathesalonike 5:17. "Yule atakayefaulu katika maisha ya Kikristo lazima akae maisha ya maombi. Hivyo ni rahisi ya kutosha ikiwa atajipangia kuwa na wakati maalum wa maombi. Mpango wa Daudi na Danieli, mara tatu kwa siku, ni mpango mzuri. Zaburi 55:17 "Jioni, asubuhi, na adhuhuri, nitalala na kuugua, naye atasikia maombi yangu." Danieli 6:10 "Hata Danieli alipojua ya kuwa yale maandiko yamekwisha kutiwa sahihi

akaingia nyumbani mwake na madirisha katika chumba chake yalikuwa yamefunguliwa, kukabili Yelusalemu, akapiga magoti mara tatu kila siku, akasali, akashukuru mbele za Mungu wake, kama alivyokuwa akifanya tokea hapo mbeleni."

Anza siku kwa kushukuru na kuomba - kushukuru kwa huruma zisizo na kipimo za wakati uliopita, omba kwa mahitaji yanayohesabika ya siku hiyo. Simama katika tiya masumbuko, na wasiwasi na majaribu ya siku ndipo uweze kutoa shukurani na maombi. Ifunge siku kwa kushukuru na kuomba.

Kisha pahitajika maombi maalum ya majaribu maalum - tunapoona majaribu yakitujia. Endelea kumtazama Mungu. "Omba bila kukoma". Huhitajiki uwe katika magoti yako kila wakati. Lakini moyo wako unahitaji uwa katika magoti kila wakati. Ikiwa "shetani hutetemeka akimwona matakatifu dhaifu akipiga magoti," natuendelee kumtetemesha kila wakati. Kwa kweli, tunafaa kuwa katika magoti yetu mara kwa mara. Haya ni maisha ya furaha, yasiyo na wasiwasi na shughuli. Hapa ndipo penye alama (za kupuuza kuomba) pale wengi huanguka.

Kunayo mambo matatu ambayo kwake ambaye atafaulu katika maisha ya Kikristo lazima hasa aombee: Kwanza, kwa ajili ya hekima, "lakini mtu kwenu akipungukiwa na hekima, na aombe dua kwa Mungu, awapaye wote kwa ukarimu" Yakobo 1:5; pili, kwa ajili ya nguvu, "bali wao wamgojeao Bwana watapata nguvu mpya," Isaya 40:31; tatu, kwa ajili ya Roho Mtakatifu, "Baba yenu wa mbinguni atawapa Roho Mtakatifu hao wamwitao." Unastahili kwa kila dharura ya kazi ya Kikristo umwombe Mungu akujaze upya na Roho Mtakatifu. Matendo ya Mitume 4:31.

5. ENENDA KUMFANYIA KRISTO KAZI: Mathayo 25:29,"Kwa maana kila mwenye kitu atapewa na kuongezewa tele, lakini asiye na kitu, hata kile kidogo alicho nacho atanyanganywa." Tazama ufunuo wa hili inamaanisha, wale hutumia kile walichonacho watapata zaidi na wale ambao huacha kile walicho nacho kikae bure hata hicho watakipoteza.

Mkristo anayefanya kazi, yule ambaye hutumia talana zake ziwe ni chache au ni nyingi, katika huduma ya Kristo, ndiye yule aendeleaye na maisha ya Kikristo hapa, na hapo baadaye atasikia "Vyema sana, mtumwa mwema na mwaminifu, ingia katika furaha ya Bwana wako.

Tafuta kazi fulani ya Kristo uifanye na uitende. Tafuta kazi. Ikiwa sio zaidi ya kuvitoa vijikaratasi vya injili au mialiko kwa mikutano, ifanye. Kila wakati kuwa ukitafuta kumfanyia Kristo kitu zaidi, na utakuwa ukipata kitu zaidi kutoka kwa Kristo.

6. TOA KWA WINGI: Mithali 11:25 "Nafsi ya mtu mkarimu itawandishwa" 2 Wakorintho 9:6,8 "Apandaye haba atavuna haba; apandaye kwa ukarimu, atavuna kwa ukarimu. Na Mungu aweza kuwajaza kila neema kwa wingi, ili ninyi, mkiwa na riziki za kila namna siku zote, mpate kuzidi sana katika kila tendo jema."

Kufanikiwa na kukua katika maisha ya Kikristo hutegemea vitu vichache zaidi ya kutoa kwa ukarimu. Mkristo mchoyo hawezi kuwa anavyoanza kuw Mkristo anayekua Ni ajabu jinsi mtu Mkristo huanza kukua anapoanza Kutoa. Toa kwa utaratibu.

Wekea Kristo kando kiwango fulani cha pesa zako zote na vitu vyote uvipatavyo. Kuwa mwaminifu na uwe mwaminifu kukihusu. Usikitumie kwa ajili yako katika hali yo yote ile. Sehemu ya kumi ni nzuri ya kuanza nayo. Usikubali iwe chini ya hiyo. Baada ya kupeana sehemu yako ya kumi, labda baadaye utajifunza furaha ya kutoa sadaka za hiari pamoja na sehemu ya kumi.

7. ENDELEA KUKAZA MWENDO): Wafilipi 3:13,14 "Ndugu, sijidhani nafsi yangu kwamba nimekwisha kushika; ila natenda neno moja tu; nikiyasahau yaliyo nyuma, nikiyachuchumilia yaliyo mbele; nakaza mwendo niifikilie mede ya thawabu ya mwito mkuu wa Mungu katika Kristo Yesu." sahau kile kilicho nyuma yako; chuchumilia mambo mema yaliyo mbele.

"Niliyachuchumilia yaliyo mbele; nakaza mwendo niifikie mede ya thawabu ya mwito mkuu wa Mungu katika Kristo Yesu." Sahau dhambi zilizo nyuma. Ukishindwa pahali., Ukianguka, usife moyo,

usikate tamaa, usiwaze juu ya dhambi. Ikiri mara moja. Amini neno la Mungu 1 Yohana 1:9." Tukiziungama dhambi zetu, yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote."

Amini kwamba dhambi imesamehewa, isahau, chuchumilia mbele. Shetani huzidanganya roho nyingi hapa. Huendelea kutukumbusha kuhusu kuanguka kwetu na dhambi zetu. Pia hutufanya tufikiri hii ni hali ya binadamu, na kama ndiyo hali ya binadamu kulitia shaka neno la Mungu na kumfanya yeye mwongo kwa kutoamini kwamba dhambi imesamehewa na kutupiliwa mbali, anaposema hivyo.

Sahau matekelezo na ushindi wa zamani na chuchumilia mbele kwa yaliyo makuu. Hapa Shetani huwadanganya wengi wetu kutoka kwa maisha makuu hutufanya tuwaze zaidi ya yale ambayo tumeshayapata kutufanya tutosheke nayo na kutuvimbisha hadi tunasimama, au pia kurudi nyuma. Kuna kitu chema mbele kila wakati hadi "tutakapofika...hata kuwa mtu mkamilifu, hata kufika kwenye cheo cha kimo cha utimilifu wa Kristo" Waefeso 4:13.

MWOKOZI NA MWENYE DHAMBI

MWENYE DHAMBI

Mshahara wa dhambi ni mauti. Warumi 6:23

Mungu unionee huruma mimi mwenye dhambi. Luka 18:13.

Nifanye nini ili niokoke? Matendo 16:30

MWOKOZI

Karama ya Mungu ni uzima wa milele. Warumi 6:23.

Kwa maana jinisi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa mwanawe pekee, ili kila amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele. Yohana 3:16.

MWENYE DHAMBI

Kwa sababu hii najichukia nafsi yangu, na kutubu katika mavumbi na majivu.

Ayubu 42:6.

Usitiri uso wako usitazame dhambi zangu. Zaburi 51:9.

MWOKOZI

Nimeyafuta makosa yako kama wingu; unirudie: maana nimekukomboa.

Isaya 44:22.

MWENYE DHAMBI

Usinitenge na uso wako, Wala Roho wako Mtakatifu usiniondolee. Zaburi 51:11.

MWOKOZI

Wote anipao Baba watakuja kwangu; wala ye yote ajaye kwangu

sitamtupa nje kamwe. Yohana 6:37.

MWENYE DHAMBI

Sisi sote kama kondoo tumepotea. Isaya 53:6.

MWOKOZI

Ni nani kwenu, mwenye kondoo mia, akipotewa na mmojawapo, asiyewaacha wale tisini na kwenda nyikani, aende akamtafute yule aliyepotea hata amwone? Naye akiisha kumwona, humweka mabegani pake akifurahi. Luka 15:4,5.

Kwa kuwa mwana wa Adamu alikuja kutafuta na kuokoa kile kilichopotea.

Luka 19:10.

MWENYE DHAMBI

Ee Bwana unijulishe njia zako, Unifundishe mapito yako. Zaburi 25:4.

MWOKOZI

Mwayachunguza maandiko. Yohana 5:39.

Kila andiko, lenye pumzi ya Mungu, lafaa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa kuwaadibisha katika haki.

2 Timotheo 3:16.

MWENYE DHAMBI

Unifumbue macho yangu nitayazame maajabu yatokayo katika sheria yako.

Zaburi 119:18.

Usinifiche uso wako, Usijiepushe na mtumishi wako kwa hasira. Zaburi 27:9.

MWOKOZI

Sitakupungikia kabisa, wala sitakuacha kabisa.

Waebrania 13:5.

Naam nimekupenda kwa upendo wa milele, ndiyo maana nimekuvuta kwa fadhili zangu Jeremia 31:3

Wanipenda? Yohana 21:17

MWENYE DHAMBI

Bwana wewe wajua yote; wewe umetambua ya kuwa nakupenda Yohana 21:17

MWOKOZI

Mkinipenda, mtazishika amri zangu Yohana 14:15 Amri Mpya nawapa, mpendane. Kama vile nilivyowapenda ninyi mpendane hivyo. Yohana 13:34

MWENYE DHAMBI

Kwa maana najua ya kuwa ndani yangu, yaani, ndani ya mwili wangu, halikai neno jema; kwa kuwa kutaka nataka, bali kutenda lililo jema sipati kwa maana lile jema nilipendalo silitendi: bali lile baya nisilolipenda ndilo nitendalo Warumi 7:18,19

MWOKOZI

Neema yangu yakutosha maana uweza wangu hutikilika katika udhaifu

2 Wakarintho 12:9.

MWENYE DHAMBI

Bwana,. tuongezee Imani Luka 17:5

MWOKOZI

Ombeni nanyi mtapewa Luka 11:9.

Maana ni yupi kwenu aliye baba, ambaye mwanawe, akimwombe mkate atampa jiwe? Luke 11:11

Basi ikiwa nyinyi mlio waovu mnajua kuwapa watoto wenu vipawa vyema, je! baba aliye mbinguni hatazidi sana kuwapa Roho Mtakatifu hao wamwombao?

Luka 11:13.

Lakini tunda la Roho ni upendo, furaha amani, uvumilivu, utu wema, fadhili,. uaminifu, upole kiasi, Wagalatia 5:22,23

MWALIKO

Unaalikwa kuitisha nakala za vijikaratasi na vijitabu vya vielelezo

Kijitabu hiki kimechapishwa na chapatikana kutoka
Revival Movement Association,
2 Clara Street,
Belfast,
BT5 5GB.,
N. IRELAND U.K.